

Mpango wa ukombozi

Waebrania 9:11-12 Lakini Kristo....kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika patakatifu. akiisha kupata ukombozi wa milele

Huo ulikuwa mpango wetu kuwa na makanisa yetu na madhehebu yetu. lakini huo haukuwa mpango wa Mungu. Tulijaribu huo bustani ya Edeni. Ulikuwa ni wa zamani kama edenii ilivyo. ‘Dini’ maana yake “ni kitu cha kujifunika.” Na Adamu alijaribu kujifunika mwenyewe kutengeneza njia yake mwenyewe. Lakini haikuweza kutenda kazi.

Kuna mahali pamoja tu ambapo Mungu atakutana na Mtu: hapo sio katika Elimu yake; sio katika Dhehebu lake, au tabaka lake :ni chini ya Damu. **Na hapo ndipo mahali pekee Mungu alipowahi au atakapo kutana na jamaa ya Binadamu, ni chini ya Damu. Hapo ndipo mahali.** Mungu aliuandaa huo utaratibu katika bustani ya Edeni ilikuwa ni kwa damu kumwagika.

Na kama Mungu atafanya uamuzi, Kamwe hawezi kuubadilisha Huo, kwa sababu Yeye ni mkamilifu, na kila anachokifanya au kukisema ni kikamilifu. Kwa hiyo hawezi kubadilisha mpango wake ili mradi ingaliko dunia na ili mradi yupo mwenye dhambi. **Kuna njia moja pekee, tangu bustani ya Edeni,** wakati dhambi ilifanyika kwa mara ya kwanza, mpaka dhambi ya mwisho itakapofanyika. **Kuna mpango wa wokovu mmoja tuu; ambao ni kupitia damu iliyomwagika.**

Hakuna chochote kiwezacho kutenda kazi. **Kanuni zetu madhehebu yetu,** na vyote vimekuwa na sehemu tena sehemu nzuri, **lakini haikuwa Ni mpango wa Mungu. Mpango wa Mungu ni kule nyuma kwenye Damu.** [1]

Madhehebu yanakiri kwamba wanaamini Damu. **Lakini wanaukataa mpango unaoturudisha kwenye Damu, Neno.** [2]

Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alisema, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno” (Yohana 1:1-3). Na Neno ni nini? Ni wazo lililodhihirishwa. **Mungu Baba, akiona mpangowa wokovu,**

aliuangualia wote na kuona kile shetani alichokifanya. Naye aliwaza, na akaona mpango pekee, ulikuwa katika wazo hapo. **Lakini alipoudhihirisha, ukawa ni Neno. Na ukiwa ni Neno kamwe hauwezi kufa;** unakuwa ni wa milele. Kwa maana Neno Lake haliwezi kushindwa kama Yeye asivyoweza kushindwa. [3]

Na Mungu, alipoona adui wa ulimwengu **vile atakavyofanya, Mungu alifikiri vile atakavyo utuma mpango ule mkuu wa ukombozi, na alipoufikiria, halafu akaunena, na ulikuwa mzuri tuu kama uliokwisha kufanyika wakati huohuo** (Mithali 8:22-31). **Na miaka elfu nyingii baadae alikuja Bwana Yesu Kristo. na akafa kwa dhambi na kufufuka tena miaka elfumoja mia tsa iliyopita kwa kuhesabiwa haki kwetu** (Isaya 9:1-7). **akiwa amekaa mkono Wake wa kuume sasa, kama kuhani mkuu akifanya upatanisho juu ya maungamo yetu** (1Tim:3:16). Unaona ni kazi iliyokwisha kukamilika, na Neno lolote litakalo katika Biblia ya Mungu. Unaweza kuipumzisha Nafsi yako juu ya hilo. [4]

Sasa, Adamu alipotenda dhambi kwa mara ya kwanza, katika bustani ya Edeni. **Mungu alikuwa na njia ya ukombozi kwa ajili yake,** kwa haraka sana baada ya yeye kukosa. Mungu alitengeneza njia ya ukombozi. Na kabla ya Adam kuweza kumkaribia tena kwenye ushirika na Baba, Mungu ilibidi achinje mwanakondoo au kondoo asiye hatia na hatia. Amfanyie nguo ya kumzunguuka. (mwanzo 3:21) na amfanyie zulia la kumkaribisha tena atembelee zulia la ukombozi, Na hiyo ni kupitia kwenye damu. Mungu siku zote ana mpango wa ukombozi, na huo ni kupitia kwenye damu, Tangu pale mwanzo na nyakati zilizofuata, ilikuwaziwa katika nia ya Mungu, kabla ya dunia kuwepo. [5]

Ilipokuja kwenye mpango wa wokovu, Alikuwa peke yake; hakuna aliyekuwa pamoja Naye. Alikuwa Ndiye pekee aliyeweza kuja. Malaika asingeweza kufanya hivyo. Mtu mwingine aitwaye mwana Wake, asingeweza kufanya hivyo. Mmoja aitwaye kitu kingine, bikira mtakatifu, au mama mtakatifu, au mtakatifu fulani asingeweza kufanya hivyo. Ilibidi Mungu aje. “Na nitawapa ishara. **Bikira atachukuwa mimba; na mtoto atazaliwa, na atakuwa Emmanueli: Mungu**

pamoja nasi.”(Isaya 7:14) ishara kuu.Mungu ndani ya watu wake. Mungu pamoja na watu wake. Mungu akawa mmoja wa watu Wake.Mungu na mtu wakawa mmoja. [6]

Kulikuwa na kitu kimoja tu ambacho hakikuanguka,**na hicho ni Mungu,zile mbingu.** Kwa hiyo kitu fulani cha mbinguni ilibidi **kije Chini kuokoa uumbaji huu,** kwa sababu hakukuwa na kitu hapa cha kuweza kuumba hiyo.**na upendo wa Mungu mwenyewe kwa watu wa ulimwengu ukaumba tabia iliyodhihirishwa ndani ya Kristo.**

Yeye alikuwa Tabia ya Mungu.Alikuwa ni sura ya Mungu iliyodhihirishwa. (kol.1:13-15).Ndani Yake alikaa Mungu. Mungu ndani ya Kristo akijifunua mwenyewe kwa ulimwengu(2Kor.5:18-19). **Na hakuna upendo mkuu uwezao kuwa mkuu zaidi ya upendo huo,** kwamba mtu kama alivyo angeweza kuwa alivyokuwa ili akomboe kile kilichopotea.(Luka 19:10).Wazo hilo tuu lingetosha kuifanya dunia yote ione aibu.kuwa tumeangukia katika mazingira gani na kile...**Mungu alichojidhihirisha mwenyewe kufanya mpango wa ukombozi kuokoa hii tabia yetu iliyoanguka.**

Hii imefanyika ili ile adhabu iweze kulipwa.Kwa sababu **adhabu ilikuwa ni mauti.** Na mmoja aliyekuwa amehukumiwa adhabu ya kifo hangeweza kulipa ile adhabu kwa mwingine aliyekuwa chini ya hukumu ya kifo.**kwa hiyo ilibidi aje mmoja ambaye alikuwa huru na mauti ili kulipa adhabu** (Waebr.2:9).Na hakuna mwingine ambaye angeweza kuja ila Mungu. Kwa sababu **alikuwa wa pekee aliyekuwa huru na adhabu ya kifo.**(Warumi 6:23). [7]

Na wakati Yesu alipokufa kwa ajili ya dhambi,**Alikufa kwa ajili ya kila kitu kilichotokea kwa sababu ya dhambi.** Unaona? Kwa hiyo swala la dhambi lilipomalizwa, lilimalizwa lote kabisa. **Mpango wote wa ukombozi**(Yohana 19:30: Wakolosai 2: 13-15).Kama unampiga yeye kichwani kwa swali la dhambi (Mwanzo 3:15).Unapouwa dhambi unauwa kila kitu ambacho kimesababishwa na dhambi. [8]

Yesu alikuwa ni ukamilifu wote wa Neno la Mungu. **Mpango wwake wote wa ukombozi, Utoshelevu wote wa Mungu ulikuwa ndani Yake** (kolosai 2:9-10). [9]

Vema mpango wote wa ukombozi uko katika hii mihuri,kitabu chote.[10]

Ile mihuri saba.**Ilikuwa imefungwa na siri saba. Na katika mihuri hii saba, ndimo hii siri yote ilimoshikiliwa,na ni kitabu cha ukombozi: Agano jipya,**siyo la zamani:lilikuwa linatangaza kule kuja kwa lile Jipya.“Hawawezi kukamilishwa Pasipo sisi.”(Waebrania 11). **Unaona,sasa ukombozi ulikuja tu pale mkombozi alipokufa.na Kimsingi walikuwa chini ya damu ya kondoo** (Waebr.10:11-22) **na siyo ya mkombozi,**Walikuwa hawajakombolewa bado mpaka mkombozi alipokuja.

Angalia sasa,Wakati mkombozi huyu....Yohana alipoangalia huku na huku,na hapa amekaa **Mungu katika kiti cha Enzi na kitabu mkononi Mwake ambacho kimefungwa na mihuri saba,na mpango wote wa ukombozi ulikuwa ndani yake**(ufunuo 5+6).

Yohana aliangalia huku na huku,na hakuonekana mtu mbiguni,hakuonekana mtu duniani,hakuna mtu. Hakuna Malaika, **hakuna chochote kilichoweza kuchukua hicho kitabu au kufungua muhuri zake au hata kukitazama.** Hakuna mtu aliyestahili.Yohana alisema alilia kwa uchungu (ufunuo 5:1-5) Ndipo Malaika akaja kwake,akamwambia “usilie Yohana ,kwa maana Simba wa kabila laYuda ameshinda Naye Amestahili”

Na Yohana aliangalia aone Simba, na aliona nini? Mwanakondoo,**aliyekuwa amejaa damu, Mwana kondoo aliyekuwa amechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ullimwengu** (ufunuo 13:8).akaja mwanakondoo, akamwendea **Yeye aliyekuwa na kitabu katika mkono wake wa kuume,na akakipokea kitabu,akapanda kwenye kiti cha enzi na kuketi.** Hilo ndilo.ilikuwa imekwisha.Lini? **Mihuri ilipofunguliwa.** Yule wa mwisho ambaye...Kila kitu ambacho amekikomboa,hakukuwa na chochote... Alikuwa kukomboa. [11]

Na sasa, tumeona kwamba Mwana kondoo aliyechinjwa amejaa damu,akitoka damu mwili wote. Alikuwa amechinjwa,Baada ya kuchinjwa,alifufuka tena na amekaa kwenye kiti cha enzi.Nyuma ya kiti cha Enzi kama hivi,akifanya upatanisho kwa nafsi zote ambazo zingemjia. **Wakati yule mmoja wa mwisho alikuwa hapa na ikakamilika...**Mungu bado anashikilia kitabu cha ukombozi. **Unaona sasa? Sasa hivi anafany kazi ya ndugu wa karibu: Kama boazi alivyoenda chini.na Ruth alikuwa tu amekaa pale mpaka Boazi...**Ninamaanisha Boazi amefanya kazi ya ukombozi ya ndugu wa karibu (Walawi 25:25-55)

Wakati mihuri hii saba ilipofunguliwa,hiyo ilifungua Biblia yote.

Sasa, Ruth alikuwa anangojea, kwa sababu amekwisha fanya kazi. Amekwisha fanya haya mambo mengine, **lakini alikuwa anangojea. Na wakati Kanisa linapokuwa linangojea, limepumzika, wengi wao Wakiwa kaika mavumbi ya dunia** (ufunuo 14:13); **wakati Yeye anafanya kazi yake ya ndugu wa karibu** (Ruth 2:4)

Sasa, anaenda kulionyesha kanisa kile alichokifanya. unaona? Halafu sasa anachukuwa... **lakini kile kitabu kimefungwa. Hakuna aliyejua hata kidogo. Wanajua ni kitabu cha ukombozi ndani pale, lakini kitafunuliwa wakati wa mwisho sawa na ufunuo 10. Malaika wa saba atapewa ujumbe wa hilo, kwa sababu imesema kwamba katika wakati atakapopiga baragumu lake katika wakati wa saba—Yule Malaika wa saba, atakapopiga baragumu yake, Siri zote za Mungu zitakuwa zimefunuliwa kwa baragumu yake. Halafu baada ya kufunuliwa, yule malaika anashuka kutoka mbinguni, ambaye ni Kristo.** (sasa kumbuka, **huyu malaika yuko duniani, Yule mjumbe**). **Kristo anashuka chini** (unamuona Yeye katika Ufunuo sura ya 10). **Anaweka mguu mmoja juu ya nchi na mwingine juu ya bahari, Upinde wa mvua juu ya kichwa chake, Macho kama—na miguu kama moto nakadhalika, akainua mikono yake na kuapa kwa Yeye aishiye milele na milele, ya kwamba hakutakuwa na wakati tena.** [12]

Sasa kumbuka huyu malaika wa saba (ufunuo 10:7) atakuwa duniani wakati wa kuja huku. [13]

Na hiki kitabu chenye sehemu saba ya mipango saba ya ukombozi kimeletwa kwetu, na hicho ndicho hiki kitabu. kinachoshikilia. Sasa tutaenda kuona katika hii sura ya 10 ya ufunuo ambapo huyu Malaika mwenye nguvu anatangaza jambo fulani, na ana kitabu kidogo ambacho Yohana alipaswa akile. Na alipokila, kikawa kichungu tumboni mwake, lakini mdomoni mwake kilikuwa kitamu (Ufunuo 10:8-11).

Unapokisaga tumboni, hapo sasa kinakuwa kichungu, kila mtu yuko kinyume na wewe, kila mtu anasema Wewe ni mtakatifu anayeviringika, wewe ni hiki, kile, au kinginecho. Unaona, huko kwenye akili zako timamu. **“kwa hiyo ni kigumu kukisaga hicho; lakini unaposhuhudia juu ya utukufu wake, ni kitamu katika midomo yako.** hivyo ndivyo ilivyo unaona? Na unaposimama katika mkutano, unasema, Utukufu kwa Mungu. Hallelujah...” Oh, wakati

unaenda katika mapambano hayo makuu, ni vigumu; lakini unapotoka katika mapambano hayo makuu unaweza kushuhudia juu ya hilo, hapo sasa ni kitamu mdomoni. Unaona? Hiyo nikweli. **Hicho ndicho kitabu cha ukombozi** [14]

Na uangalie vile Mungu anavyoweza wazi kwetu mpango Wake wa ukombozi. Oh, hilo nilipoliona liliwasha moyo wangu moto. Jinsi anavyoweza wazi hapa, **mpango Wake wa ukombozi.** Sasa linganisha na kile tunachokiona na macho yetu **Kile Mungu amefanya kukomboa dunia Yake. Amefanya mpango huohuo kukomboa watu wake. Kwa maana Mungu asiyebadilika habadilishi chochote kile katika mpango wake au Chochote. Jinsi kilivyo cha utukufu.**

Angalia dunia ya kale (wakati wa gharika), dunia ambayo iko sasa, na ile nyingine ijayo. Sasa hatua ya kwanza ambayo Yeye anatuleta kuifikia... Unaona. **Mpango wake wa ukombozi unafanana kwa kila kitu. Anatumia njia ileile.** Kamwe habadiliki. Alisema katika Malaki 3:6. “Mimi ni Mungu sibatiliki.” Namna anavyolifanya. Kwa hiyo, **kama aliokoa mtu wa kwanza aliyewahi kuokoa kwa damu iliyomwagika ya kimoja kisichokuwa na hatia, Itabidi aokoe kingine vivyo; na kila kimoja Atakacho okoa itabidi afanye vivyo hivyo.** Kama ameponya mtu wakati wowote katika safari ya maisha, iwe katika siku za Yesu, za mitume, za manabii, vyovyote ilivyo, wakati mazingira yakifanana inaidi alifanye hilo tena. Hiyo ni kweli. Yeye habadiliki. **Watu wanabadilika, muda unabadilika, Nyakati zinabadilika, Vipindi vinabadilika, Lakini Mungu yule Yule: mkamilifu.** Hiyo inapaswa kuwapa tumaini kuu wale walio wagonjwa.

Kama aliwahi kuponya mtu, mgonjwa anapaswa kufanya hivyo hivyo tena wakati hali zikifanana. Aliwahi kuokoa mtu, Anapaswa kulifanya hilo katika msingi uleule Aliolifanya wakati wa kwanza. Kama aliwahi kumjaza mtu na Roho Mtakatifu, Anapaswa kulifanya tena katika msingi uleule alipolifanya mara ya kwanza. Kama aliwahi kumfufua mtu kutoka kaburini. Inabidi alifanye hilo tena mara ya pili na wakati mwingine wowote katika msingi uleule. Yeye habadiliki.

Kumetokea nini? Kristo alikuja na kuliita Kanisa lije kwenye

toba.(Maji) ubatizo kwa Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi,akalitakasa Kanisa,na kwa moto wa Mungu alikuja chini na akateketeza uchafu wote na kuja kukaa katika moyo wa mwanadamu (Matendo 2: 37-41).

Sasa, **Dunia ,inaokolewa kwa ajili ya mtu huyu aliye Kombolewa. Anatomia njia Yake ileile.** Aliibatiza katika maji baada ya maangamizi (ya wakati wa Nuhu).Alimwaga Damu Yake ili kuitakasa na kuidai. Ni mali Yake.

Unaona shetani hapa katika maandiko alivyojaribu kumfanya avunje mpango wa Mungu kwa kuipokea—alimpaYeye.Pale alipomchukua Yeye(Yesu) kule juu ya mlima.**Na akajaribu kumpa Yeye hiyo bila kuinunua kwa Damu?(Luka 4:1-13).**

Shetani alijaribu kumwambia kuwa,“ nitakupa wewe hiyo” Naye akasema hapana.bwana. Na iwe ni shahidi. Aliinuliwa juu kama ishara--kwamba Ameinunua. Ameigharimia hiyo. Lakini sasa inabidi ipitie ubatizo wa moto(ufunuo 21:1),moto mtakatifu kutoka kwa Mungu ambao unaisafisha dunia na mbingu zinoyoizunguka.Hapo sasa iimenunuliwa ili kwamba waliokombolewa waishi ndani yake—waishi ndani yake kwa amani.

Angalia, **ubatizo wa moto ni kwa ajili ya kuitakasa kutoka dhambi,kutoka magonjwa, wadudu wa magonjwa,kutoka kwa wenye dhambi,kutoka kwa shetani na kundi lake lote .**

Yeye atatupwa na kwenye ziwa la moto(ufunuo 20: 10) **moto Mtakatifu kutoka kwa Mungu unashuka chini kutoka kwa Mungu Mbinguni nakuichoma hiyo ili kuifanya tayari kwa Mungu kukaa ndani yake.** Kwa maana katika ulimwengu mpya ujao, Mungu atakaa Duniani kwa sababu...Unasema, “Mungu? **Anakaa katika moyo wa binadamu.”** Lakini Yeye na Bibiarusi wanakuwa Mmoja, na wanaenda kwenye nyumba yao katika ulimwengu ule mpya.(ufunuo 21:2-14).**Na mpango uleule wa ukombozi unatumika Kukomboa wote dunia na watu watakaokaa ndani yake.**

Unaona, moyo unabidi utakaswe kama hivyo.**Kabla ya Mungu kuja chini katika utu wa Roho Mtakatifu,ambaye ni Kristo akija chini na kukaa katika moyo wa Mtu, lazima kwanza utubu** (Matendo 3:19-21).**Lazima ubatizwe katika maji kwaJina Lake kuonyesha kuwa ni mali ya nani** (Matendo10:47-48).

Halafu ni lazima itakaswe kwa damu yaYesu (1Yohana1: 7; Waeb.9:14).Na halafu moto mtakatifu na Roho Mtakatifu kutoka kwa

Mungu unakuja chini na kuchoma kabisa tamaa zote za dhambi,tabia zote za dunia (matayo 3: 11).

Unaona, Yeye anakomboa dunia kwa namna ileile Anayo Komboa watu Wake. Anafanya hayo yote kwa namna ileile, Mpango wake wa ukombozi. Kwa maana ni Mungu asiyebadilika, siku zote Yuko vilevile katika mpango wake. [15]

Kutoka mwanzo mpaka ufunuo,mpango kamili wa ukombozi unafunuliwa katika hii mihuri. oh, ni wakati wa muhimu. Mungu atusaidie kulipata hilo. [13]

Nukuu za kiingereza:

- [1] Sauti zisizokuwa za uhakika (61-0315).aya1-28
- [2] Lile shitaka aya 101
- [3] Mungu anashika Neno Lake (57-0120E).aya 1-26
- [4] Mshindi Mkuu (56-0401).
- [5] Mtumishi wa Mungu Ayub (55-0223).aya E-19
- [6] Ishara Kuu (59-1227M). aya 77
- [7] Kitambulisho (63-0123). Aya E-22
- [8] Mungu atajipatia 2 (60-0802).aya E-19
- [9] Karamu ya Baragumu uk.11-6
- [10]Mhuri wa sita Ktb cha mihuri uk.436
- [11]Roho zilizoko Kifungoni sasa uk.24-25
- [12]Mhuri wa tatu ktb cha Mihuri uk.234-235
- [13]Lile Pengo ktb cha Mihuri uk.74-2,92-2
- [14]Ufunuo Sura ya 5 sehemu ya 2 aya 100-102
- [15]Makao ya Baadae uk.14-15,17-18,19.

iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306.

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa: Charles E. Y. Kanju,
Box 5138, Tanga
E-mail: chaelika@hotmail.com
Cell.phone 0784704299*